**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA**
**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE 2021/2022.**

S.L.P. 228,
MPANDA-KATAVI.
**Website: w.w.w.mpandasec.sc.tz**
**0755247496/0757533898**
**18/03/2022.**

Tafadhali unapojibu taja:
**Kumb.Na:MG/ADM/09/1988/…….**
Ndugu……………………………………
………………………………………….
………………………………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA KIDATO CHA TANO MWAKA WA MASOMO 2022/2023.**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari ya Wasichana Mpanda mwaka 2022. Shule hii ni ya **bweni na ni ya wasichana**. Shule **ipo Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, katika Wilaya ya Mpanda Mkoa wa Katavi**.

Tafadhali wahi kufika maana **ukichelewa zaidi ya wiki mbili (2)** nafasi yako itachukuliwa na mtu mwingine. Shule itafunguliwa muhula wa kwanza na mwisho wa kuripoti itakuwa ni wiki mbili tangu shule kufunguliwa.

Hongera kwa kuchaguliwa katika Shule hii, nakutakia maandalizi mema na safari njema, karibu sana Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda.

…………

**NYABISE M. SABASI**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda
S. L. P. 228 Tel; 2820295 MPANDA

**YAFUATAYO NI MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE HII AMBAYO NI MUHIMU UYAFUATE:**

## A. USAFIRI

Kila mwanafunzi atajitegemea usafiri. **Usafiri wa gari moshi toka Tabora kuja Mpanda** upo kila **Jumatatu**, **Jumatano** na **Jumamosi**, na gari moshi hufika Mpanda siku za **Jumanne**, **Alhamisi** na **Jumapili**. Pia usafiri wa mabasi upo kila siku. Usafiri wa **mabasi** kutoka **Mbeya hadi Mpanda**, unapatikana kila siku kwa mabasi ya **Ruchoro Express, Nyasa, na Big Sam**. Kutoka **Arusha mpaka Mpanda** kuna mabasi ya kampuni mbili tu ambazo ni **Coast line na Mumuk**. Kutoka **Mwanza hadi Mpanda** kila siku kuna **Fikoshi**, **ALLYS, KISALE,NBS na Primier line**. Na kutoka Kigoma kuna mabasi ya kampuni za **Adventure Connection, Saratoga, Ruchoro express na Superdoll**. Pia kuna usafiri wa **Ndege za kampuni ya ATCL** ambazo hufanya safari zake siku za **Jumanne, Alhamis** na **Jumamosi** kutoka **Dar es Salaam** kuja **Mpanda.**

**Ukifika Mpanda**:

(I). Kutoka stesheni ya Gari moshi, Shule iko magharibi, umbali wa km 4.

(II). Kutoka kituo cha mabasi (Stendi kuu ya Mizengo Pinda) shule iko magharibi umbali wa km 8 usafiri wa **Tax** na **Bajaj** unapatikana.

**NB:** Kutokana na maazimio ya kikao cha wazazi kilichoketi kuangalia maendeleo ya shule, pamoja na mambo mengine iliamuliwa kuwa wanafunzi watasindikizwa na walimu wakati wote wa kwenda nyumbani likizo na wanaporudi shuleni baada ya likizo kuisha. Hivyo kwa atakayehitaji kuambatana na magari haya awasiliane na mwalimu msaidizi wa usafiri kwa namba zifuatazo:- **0762336233**, **0787695723** au **0675485286 Mwl. Safari Masasi** (kwa magari yanayoanzia safari Tanga, Arusha, Mwanza na Dar es salaam), na **Mwl. Jofrey Jonathan Mtweve 0765082888** (kwa magari yanayoanzia safari Ruvuma na Iringa kupitia Mbeya na Rukwa

## B. VITU MUHIMU VYA KUJA NAVYO: -

### I. SARE ZA SHULE:

a) i). Sare ya darasani ni sketi ya kitambaa cha kimasai ambayo ni lazima iwe ndefu kufika kwenye kifundo (ankle) cha miguu ya mwanafunzi. Sare hii itashonwa shuleni.

ii). Mashati mawili meupe ya mikono mirefu na yasiyo na urembo wowote.Aje nayo mwanafunzi.

iii). Kwa waislamu watashona nusu kanzu nyeupe mbili ambazo ni ndefu kidogo ikiambatana na hijjabu nyeupe mbili ndefu kidogo (kitambaa cha halua). Aje navyo.

iv). Nusu kanzu nyeupe ya mikono mirefu, ambayo itatumika kwa matukio maalum. Ataikuta shuleni.

b). Sare ya michezo ni sketi ya Blue bahari, fupi pamoja na fulana ya collar ya rangi ya njano yenye nembo ya shule. Atavikuta shule.

c). Sare ya kushindia (shamba dress) ni sketi ndefu ya rangi ya ugoro pamoja na nusu kanzu ya draft/chekechea rangi ya ugoro. Atavikuta shuleni.

d). Sweta la shule ni rangi ya kijani ya jeshi lenye nembo. Atalikuta shuleni.

e). Truck suti ya shule ni dark blue. Aje nayo.

f). Fulana ya shule ni dark blue yenye collar na nembo ya shule. Ataikuta shuleni.

NB***: Si jukumu la shule kushona sare za wanafunzi, mwanafunzi mhusika ataelekezwa kwa mtu aliyeteuliwa na shule kwa kazi hiyo, utaratibu huu umewekwa ili wanafunzi wawe na sare zinazofanana. Hivyo jumla ya gharama ya sare zote ni Tsh. 124,000/=, aje nazo mkononi.***

**NB: MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA MAVAZI YA AINA YOYOTE ZAIDI YA SARE ZILIZOTAJWA HAPO JUU.**

## II. ADA NA MICHANGO MUHIMU YA SHULE: -

| NA. | MCHANGO | MALIPO KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya shule | Tsh. 70,000.00 (anaweza kulipa Tsh. 35,000/= kwa muhula mmoja) |
| 2. | Taaluma | Tsh. 20,000.00 |
| 3. | Huduma ya kwanza | Tsh. 10,000.00 |
| 4. | Vibarua | Tsh. 30,000.00 |
| 5. | Ukarabati | Tsh. 15,000.00 |
| 6. | Godoro (Atalikuta shuleni). | Tsh. 20,000.00 (Kukodisha kwa mwaka) |
| 7. | Tahadhari | Tsh. 5,000.00 |
| 8. | Nembo | Tsh. 2,000.00 |
| 9. | Kitambulisho | Tsh. 6,000.00 |
| | **JUMLA** | **Tsh. 178,00.00** |

**YAFUATAYO YAZINGATIWE WAKATI WA KULIPIA MICHANGO.**

1. Ada na michango yote iliyoorodheshwa hapo juu, ilipwe Benki ya **NMB** kupitia akaunti namba **61901100009**.Jina la akaunti **MPANDA GIRLS SECONDARY SCHOOL**.**Isipokuwa**
2. Fedha ya **ukarabati** ilipwe kwenye akaunti namba **61901200112(NMB)** Jina la akaunti **MPANDA GIRLS SECONDARY SCHOOL DEVELOPMENT.**
3. Aje na fedha kwa ajili ya bima ya afya (NHIF) **Tsh. 50,400/=** i**lipwe mkononi wakati wa kuripoti shuleni kabla ya kusajiriwa. Fedha hii ni lazima ilipwe mhula wa kwanza. Hii inasaidia kuepukana na changamoto za matibabu ya mtoto awapo shuleni, na hata atakapo kuwepo nyumbani bima hiyo itamsaidia. Hii ni kwa wanafunzi wasiokuwa na bima ya Afya.**
4. Naomba izingatiwe kuwa Michango yote ianze kulipwa kuanzia tarehe **01/07/2022** na kuendelea (Hii ni kutokana na mifumo ya fedha ya serikali).
5. Fedha ikilipwa lazima mwanafunzi/mlezi/mzazi achanganue nyuma ya fomu ya kulipia **(Bank pay -in-slip)** michango aliyolipia, na pia nyuma ya pay-in-slip lazima liandikwe jina la mwanafunzi pamoja na tahasusi anayosoma.
6. Fomu ya kulipia benki **(sehemu ya jina la mlipaji**) lazima liandikwe jina la mwanafunzi na sio jina la mlipaji kama sio mwanafunzi.

7. Fomu ya kuwekea fedha (Bank pay in-slip) ni lazima iletwe shuleni wakati wa kuripoti.
8. Michango iliyoorodheshwa pekee ndio ilipwe benki na sio vinginevyo.
9. Hakuna michango iliyoelekezwa kulipwa benki, itakayopokelewa shuleni. Michango yote ilipwe kwenye akaunti zilizoelekezwa hapo juu katika benki ya **NMB PLC**. Benki ya NMB PLC ipo kila makao Makuu ya Wilaya, unaweza kulipa katika tawi lolote la NMB PLC.

**NB: NYUMA YA BANK PAY IN SLIP UANDIKE MAJINA YA MWANAFUNZI NA MCHANGANUO WA MALIPO HUSIKA NA KUWASILISHWA SHULENI WAKATI WA KURIPOTI. FEDHA TASLIMU HAZITAPOKELEWA, ISIPOKUWA ZILIZOELEKEZWA HIVYO.**

**III. MALAZI: -**

a) Shuka jozi mbili rangi ya kijani kibichi.
b) Mto na foronya ya rangi ya kijani kibichi.
c) Blanketi moja rangi yoyote.
d) Shuka nzito moja rangi yoyote.
e) Aje na **Chandarua ya pembe nne rangi nyeupe**.

**IV. VITENDEA KAZI: -**

1 (a)Mchepuo wa sayansi(PCB,CBG na PCM),waje na,

- Ndoo ndogo mbili(2),Vyekeo moja lililo nolewa,Jembe moja na mpini wake,Mifagio miwili(2) aina ya chelewa na Brush ngumu moja.

(b) Mchepuo wa Sanaa (HGK, HKL na HGL),waje na,

- Jembe moja na mpini wake,Mifagio miwili(2) aina ya chelewa,Brush ngumu moja,ndoo mbili ndogo,na Sweeper moja.

(c) Mchepuo wa Biashara(EGM,ECA na HGE),waje na,

- Jembe moja na mpini wake,Mifagio miwili(2) aina ya chelewa,ndoo ndogo mbili,Soft Brush moja na Panga moja lililo nolewa.

2.Madaftari makubwa (counter book Quire 3) yasiyo pungua kumi (10)

3.Daftari ndogo aina ya msomi,zisizopungua kumi(10)

4.Mathematical set, Kalamu za wino, penseli, rula, scientific calculator n.k.

5.Rim A4 mbili (02).

**V. TAALUMA: -**

Kwa kuwa shule ina uhaba wa vitabu, inashauriwa mwanafunzi aje na vitabu vitakavyomsaidia kwa masomo husika kati ya vilivyoorodheshwa hapa chini:-

**I. VITABU VYA KEMIA: -**

1. Jain s.k (2006) *Conceptual Chemistry XI ,4th edition*. Chand, New delhi India
2. Ngaiza lusima (2014) *Atomic Structure and Bonding*. Hopegen company ltd. Dar es salaam. Tanzania
3. Ngaiza lusima (2014*) Physical Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania
4. Ngaiza lusima (2014) *Inorganic Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania

5. Ngaiza lusima (2014) *Environmental and Soil Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania.
6. E. Ramsden (2001) *Calculations for A-level chemistry*.

**II. VITABU VYA BIOLOJIA: -**

1. Gleen and Toole (1999). *Understanding Biology 4th Edition*.Stanlye Thomes LTD UK.
2. Kent M. (2013). *Advanced Biology*.Oxford University Press LTD 2nd Edition
3. Aggarwal S. (2017). *A text book of CBSE.Biology for Class XI*.Nijra Publishers and Printers PVT.LTD
4. Verma P. S and Pandey BP (2012). *S. Chands Biology for class VI*.Chand and Company LTD.New Delh
5. Verma P. S and Pandey BP (2012). *S. Chands Biology for class VII*.Chand and Company LTD.New Delh
6. Taylor etal (1997) *Biological Science.3rd Edition,* Cambridge university Press LTD.
7. T.I.E (2019) *Biology for Advanced Level Secondary School.Student's Book Form Six,* Dar es salaam, T.I.E
8. T.I.E (2019) *Biology for Advanced Level Secondary School.Student's Book Form Five,* Dar es salaam, T.I.E

**III. VITABU VYA HISTORY: -**

1. Bigirwamungu, J & Deogratias M. (2015) *Understanding African History*,Paper 1, New Version, Mikumi Publishers.
2. Kato, A.K. (2012) *Mastering Advanced Level History Book*, Mwanza, Mweas Book Publishers
3. Kato, A.K (2012) *Mastering Advanced Level History Book 2,* Mwanza, Mweas Book Publishers
4. Samwel, S & Stephen. O (2008) *World History Advanced Level*, Dar es salaam, Nyambari Nyangwine Publishers.
5. Shibitali, C.K (2017) *Contemporary Historical Events,* Third Edition, Dar es salaam, Che Guevara Investment.
6. Yassin,S.(2015) *Essentials in Advanced Level History Paper 1*, Dar es salaam, Ahmaddiya Printing Press.
7. Yassin,S.(2015) *Essentials in Advanced Level History Paper 2,* Dar es salaam, Ahmaddiya Printing Press .
8. Tanzania Institute of Education (2010) *History for Secondary Schools Form Five*, Dar es Salaam, T.I.E.
9. Tanzania Institute of Education (2010) *History for Secondary Schools,* Form Five, Dar es Salaam, T.I.E

**IV. VITABU VYA KISWAHILI**: -

1. Masebo, J.A & Nyangwine. N (2010) *Tahakiki Kidato cha 5& 6.* Nyambari Nyangwine Publisher, Dar es Salaam.

2. Mwansoko, H.J.M (1996) *Kitangulizi cha Tafsiri*, TUKI – Dar es Salaam.

3. Kihore. Y.M na Wenzake (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*; TUKI Dar es Salaam.

4. Massamba, D.P.B na Wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*; TUKI Dar es Salaam.

5. Saluhaya, M.C (2010) *Nadharia ya Lugha Kidato cha 5 & 6.* S.T.C Publishers- Dar es Salaam.

6. Masebo.J.A & Nyangwine, N (2009) *Nadharia ya Lugha kidato cha 5 & 6* . Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.

7. Masebo, J. A & Nyangwine, N. (2008) *Nadharia ya Fasihi Kidato cha 5 & 6*, Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.

**V. VITABU VYA UCHUMI: -**

1. C.M. Ambilikile – *Advanced level paper two and professional studies*

2.Economic 2*; Advanced levels paper two and professional studies*

*3.Undestanding Economics* (Remed H. Chegee.M)

**VI. VITABU VYA PHYSICS: -**

1.Mehta, R. and V. K Mehta (2009) *"Principles of Physics for Class XI*" New Delhi, S.Chand and Company Ltd.

2. Nelcon, M and P. Parker (1995) *"Advanced level Physics''* 07th Edition, London, Heinmann Educational books.

3. TIE (2019) "*Physics for Advanced Level Secondary Schools*, Form Five, Dar es salaam, TIE.

**VII. VITABU VYA ADVANCED MATHEMATICS**

1.Mathematics, For Class XI, Volume I, S. CHAND

2.Mathematics, For Class XI, Volume II, S. CHAND

3.Mathematics, For Class XII, Volume I, S. CHAND

4.Mathematics, For Class XII, Volume ii, S. CHAND

5.Pure Mathematics 1, 3rd edition, Backhouse, J.K, Houldsworth, S.P.T, B.E.D(1985)

6.Pure Mathematics 2, 3rd edition, Backhouse, J.K, Houldsworth, S.P.T, B.E.D(1985)

**VIII. VITABU VYA JIOGRAFIA: -**

1. Pritchard J.M. (1979*) "Africa a study Geography for Advanced students"* London, Longman.

2.Msabila D. T (2003) *"Success in Geography climatology and Soil Science",* Dar es salaam, Afroplus Industries L.T.D

3. Prichard J.M. (1990) *"Practical Geography for Africa"* Longman.

4. Kamili, 2, *Physical Geography for Africa*, Dar es salaam, Afroplus Industries.

5.Msabila D.T. *Physical Geography*, Dar es slaam Nyambari Nyangwine Publishers.

6 Msabila D.T. (2006) *Human and economic Geography* (Advanced level paper 2) Nyambai Nyangwine publishers.

IX**. VITABU VYA SOMO LA KIINGEREZA**

1. Ndambo,G.S & Kinunda, J.E. (2017). *Advanced Level English Language 1*, Form 5&6. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
2. Kadeghe, M. (2010), *The Real English Textbook for Advanced Level,* Form Five, Dar es salaam, Jamana Printers Limited.
3. Kadeghe, M. (2010) *The Real English Textbook for Advanced Level,* Form Six. Dar es salaam, Jamana Printers Limited.
4. Asheli, N. (217) *Advanced Level English Language Structure & Stylistics*, Dar es salaam, APE publishers Ltd.
5. Lyi Kwei Armal, *the beautiful one are not yet born.*
6. Chunua Achebe, *A man of the people*
7. Heinrich Ibsen, *An Enemy of the people*
8. Ngungi wa Thiongo, *I will merry when I want*.

**X. VITABU VYA ACCOUNTANCY.**

1.Wood.F & Sangster (2018) *"Business accounting"* 14th edition, UK, Pearson publishers.

2.Saleem, N. A (2012) *"Advanced Financial Accounting Simplified*" Volume II, Nairobi.

3.Saleem N.A, (2014) *"Accounting Simplified"* latest edition, Nairobi,

4. Goyar V.K, (2014) *"Financial Accounting"* Kalyani publishers

5.Chandi S & Pillai Bagavathi (2012). *"Fundamentals of Advanced Accounting"*, Delhi publishers.

**XI.VITABU VYA COMMERCE**.

1. Saleemi, N.A (2014) *Commerce Simplified for East Africa*, Rvised and Updated, Nairobi, Saleemi publications Ltd.

**XII. GENERAL STUDIES: -**

1. Bigirwamungu, J & Deogratias M.5th Edition (2019) *Understanding Advanced Level General Studies,* Dar es salaam, Mikumi Publishers.
2. Tanzania Institute of Education (2010), *General Studies for Secondary Education*, Dar es Salaam, T.I.E

**XIII. VYOMBO VYA CHAKULA: -**

a) Sahani na kijiko.

b) Kikombe na bakuli.

**XIV. MWANAFUNZI LAZIMA AJE NA 'RESULTS SLIP' HALISI YA MATOKEO YAKE YA KIDATO CHA NNE, NA SIO KIVULI. ASIPOKUJA NAYO HATAPOKELEWA.**

**C. FOMU ZIFUATAZO ZIMEAMBATANISHWA NA NI MUHIMU KUZIKAMILISHA.**

1. Historia ya wazazi na mtoto
2. Kukubali kujiunga na shule
3. Fomu ya kupima afya (medical examination).

**TAFADHALI NI MUHIMU SANA KUPIMA AFYA YAKO NA KUJA NA VYETI ILI KUONDOA USUMBUFU**

**MWISHO: -**

Shule hii inathamini **Umoja, amani** na **juhudi katika masomo na kazi za nje**. Nidhamu safi ni msingi wa mafanikio ya kila binadamu hivyo kila atakayekubali kujiunga na shule hii atatakiwa kuzingatia maelekezo hayo. Sheria za Shule zimeambatanishwa, zisome kwa makini na uwe tayari kuzifuata.

**"MAISHA NI KUJIFUNZA"**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA**

**KIAMBATA ‘A’**

## SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA

**Kumbukumbu Namba: MG/ADM/09/1986…………**

## HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII: -

### A. WAZAZI/WALEZI

1. Jina la Baba ………………………………………………… Hai/Si hai.
2. Jina la Mama …………………………………………… Hai/ Si hai.
3. Kama Baba si hai jina la mlezi ni ……………………………………………………….
4. Kazi/Shughuli ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………….
5. Anwani ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………
6. Uraia wa wazazi
   -Baba Mtanzania/Si Mtanzani.
   -Mama Mtanzania/ Si Mtanzania.
7. Wakati wa likizo mtoto/Mwanafunzi anatakiwa arudi nyumbani kwao alikotoka ambako ni ………………………………………………………………………
8. Jina la mtu aendako ……………………………………………………….
9. Uhusiano na mtoto/mwanafunzi………………………………………….

**SAHIHI YA BABA/MLEZI………………………………………TAREHE ………………….**

**SAHIHI YA MWANAFUNZI …………………………………. TAREHE …………………**

**KIAMBATA 'B'**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by a medical officer in respect to all form of entrants
Student's full name ……………………………………………………………………………….
Age …………………………………… Years ……………………… Sex ………………….
Blood count (red and whites) ……………………………………………………………….
Stool examination ……………………………………………………………………………….
Urine analysis
Syphilis and other venereal diseases test ……………………………………………
………………………………………………………………………………………T.B test
……………………………………………………………………………
EyeTest……………………………………………………………………………
Ears…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
Abdomen……………………………………………………………………… Urine for plant test…………………………………………………………………
Test for pregnancy ……………………………………………………………………………….
ADDITIONAL INFORMATION
Defects, impotents (e.g. arms, legs etc) infections, chronic or family diseases etc
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
I certify that the named above is fit to pursue further studies in agricultural/domestic education
Station ……………………………………………….................. Signature …………………
Date.……………………………………………designation………………………………….

**KIAMBATA ‘C**

## SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

Mimi ………………………………………………………………………… nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu kuingia shule ya Sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache.

Hivyo nakubali kujiunga na shule ya Mpanda Sekondari ya Wasichana. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhi/heshima ya Shule ya Mpanda Sekondari ya Wasichana na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shuole.

Tarehe …………………………...          Sahihi ya mwanafunzi……………………………………………

Mimi Mzazi/ Mlezi …………………………………………. Nimeshuhudia mtoto wangu …………………………………….. akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea binti yangu naamini tutakuwa tunawasiliana.

Tarehe………………………………… Sahihi ya Mzazi/Mlezi…………………………………………

**KIAMBATA ‘D’**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA MPANDA**

## SHERIA ZA SHULE

### 1. UTANGULIZI.

Shule ya sekondari ya wasichana Mpanda imejiwekea malengo ya kumuandaa mhitimu wake kuwa na uwezo wa kujitegemea baada ya kukamilisha mzunguko mzima wa elimu ya sekondari. Mwanafunzi awapo shuleni atajifunza mambo mbali mbali yahusuyo stadi za Maisha. Kwa mantiki hiyo basi, kauli mbiu **(MOTTO)** ya shule yetu ni **“MAISHA NI KUJIFUNZA”.** Kama umeridhia kujiunga na shule hii, **huna budi kuitafakari kauli mbiu hii na kuichukulia kwa uzito unaostahili**. Ilikufikia malengo yetu shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa. Sheria na Kanuni hizi zinazingatia misingi ya **UTU, HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII** na **TABIA NJEMA** kwa ujumla.

### 2. MIPAKA YA SHULE

a) Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea vijiji jirani wala kwenda mjini bila kupata kibali cha Mkuu wa Shule.
b) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba za wafanyakazi wa shule bila idhini ya Mkuu wa Shule au mamlaka iliyokasimishwa madaraka hayo.
c) Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana maeneo ya idara za masomo baada ya saa 12 jioni.

### 3. MAVAZI RASMI YA SHULE

#### I. DARASANI: -

a) Sketi ya kitambaa cha kimasai ndefu inayovuka magoti na shati jeupe la mikono mirefu. Kwa mwanafunzi wa kiislamu anatakiwa kuvaa sketi ndefu na kanzu fupi nyeupe na hijjub nyeupe.
b) Viatu vyeusi simple visivyo na kamba na visigino virefu na visiwe vya kugonga
c) Soksi jozi moja nyeupe fupi itakayovaliwa darasani na jozi nyingine nyeusi itakayovaliwa na shamba dress (nguo za kushindia).

#### II. KAZINI.

Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sketi ya rangi ya ugoro (brown) na nusu kanzu ya rangi ya brown.

**III. MICHEZONI.**

Mwanafunzi awapo michezoni avae sketi ya rangi ya bluu bahari, fulana ya njano yenye nembo ya shule na raba nyeusi.

**IV. NJE YA SHULE.**

Mwanafunzi akiwa nje ya Shule avae sketi ya kitambaa cha kimasai na fulana ya rangi ya dark-blue yenye nembo ya shule na viatu vyeusi. Kwa waislamu wavae sketi ya kitambaa cha kimasai, nusu kanzu ya rangi ya ugolo na hijjab.

**V. SAFARINI.**

Mwanafunzi anapokuwa safarini avae sketi ya kitambaa cha kimasai pamoja na fulana ya shule ya dark blue yenye nembo.

**4. UTARATIBU KATIKA BWALO LA CHAKULA.**

a) Ni muhimu kufuata utaratibu, na saa zilizopangwa za kula kufuatana na ratiba ya shule
b) Kila mwanafunzi awe na sahani, bakuli, kijiko na kikombe.
c) Wanafunzi wakae mezani wakati wa chakula.
d) Wanafunzi hawaruhusiwi kupiga kelele wakati wa chakula.
e) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na Kanda mbili/ndala au kiatu cha wazi ndani ya bwalo la chakula na jikoni.
f) Mwanafunzi haruhusiwi kuhifadhi wala kupeleka chakula bwenini au madarasani.

**5. JIKONI.**

a) Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia jikoni wala kujipikia vyakula kama wanavyotaka. Viranja wa zamu na viongozi wa meza ndio wanaoruhusiwa kuingia jikoni.

**6. MABWENINI.**

a) Wanafunzi hawaruhusiwi kulala wawili kitanda kimoja.
b) Kila mwanafunzi ni lazima alale katika bweni na chumba alichopangiwa.
c) Wanafunzi hawaruhusiwi kuongea, kutembea mabwenini au nje ya bweni baada ya saa 6:00 usiku.
d) Ni marufuku kupiga na kusikiliza muziki bwenini
e) Upotevu/uharibifu wowote wa mali ya umma bwenini utalipwa na wakazi husika wa bweni.
f) Mwanafunzi haruhusiwi kuwepo bwenini wakati wa masomo au wakati ratiba ya shule ikiendelea.
g) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na chakula au kula chakula bwenini.
h) Kila mwanafunzi azingatie usafi wa bweni siku zote na siku maalumu za usafi.

**VI. DARASANI.**

a) Wanafunzi wawe madarasani mnamo saa moja na dakika ishirini (1:20) asubuhi.
b) Mwalimu anapoingia darasani wanafunzi wasimame na kumwamkia mwalimu.
c) Wanafunzi wasipige kelele wawapo darasani.
d) Wanafunzi wasitoke nje ya darasa wakati wa masomo bila ruhusa maalumu.

e) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujibu na kuuliza maswali na kukamilisha kazi alizoachiwa na mwalimu wa somo.
f) Usafi wa darasani ni wajibu wa kila mwanafunzi.
g) Upotevu au uharibifu wowote wa mali ya umma darasani utalipwa na wanadarasa husika.
h) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na chakula au kula darasani.

**7. NJE YA DARASA.**

a) Wanafunzi wasimamae na kumsalimu mwalimu au mtu aliyewazidi umri anapopita.
b) Wanafunzi wawaheshimu wafanyakazi wengine waliopo shuleni kama inavyostahili.
c) Wanafunzi watumie lugha ya heshima kwa walimu, watu wengine na hata wao kwa wao.
d) Wanafunzi wawe watii, wasiwe wagomvi, wasengenyaji, wavivu, walevi na wazururaji.
e) Wanafunzi wawe na moyo wa kushirikiana na kusaidiana wakati wa shida na raha.
f) Wanafunzi waheshimu bendera ya taifa na ukumbi wa mikutano.
g) Wanafunzi hawaruhusiwi kusomea nje ya madarasa, na mabwenini.
h) Mwanafunzi ataongea kiingereza wakati wote awapo shuleni.
i) Mwanafunzi aheshimu kengele, awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa.

**8. MATIBATU.**

a) Wagonjwa wote watatibiwa katika zahanati ya shule, na wanaohitaji matibabu zaidi, katika hospitali ya serikali tu (na si Kituo binafsi)
b) Shule haitagharamia matibabu kwa mwanafunzi. Gharama ya matibabu itagharamiwa na mfuko wa bima ya Afya ya Taifa (NHIF) kwa wanafunzi waliolipia na kupewa kadi. Kwa mwanafunzi asiye na bima ya NHIF atapaswa kugharamiwa matibabu na mzazi/mlezi wake.

**9. MAKTABA YA SHULE.**

a) Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia maktaba wakiwa wamebeba mikoba ya vitabu/ madaftari.
b) Wanafunzi waingie maktaba wakiwa wamevaa vazi rasmi la shule.
c) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya maktaba na kitabu au gazeti bila ruhusa ya mkutubi au mwalimu mhusika na maktaba
d) Mwanafunzi ataingia maktaba katika muda maalumu uliopangwa.

**10. WAGENI.**

a) Wageni wa aina yoyote ile hawaruhisiwi kuingia au kupita shuleni bila shida maalumu na idhini ya mlinzi wa zamu.

b) **Wageni** wa aina yoyote ile hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi isipokuwa kwa wale wenye shida za kiofisi tu.

c) Maagizo yote ya wageni kwa mwanafunzi au wanafunzi yatapokelewa na mwalimu wa zamu **(vyakula, vinywaji na dawa havitapokelwa).**

**11. HUDUMA ZA OFISI.**

a) Ofisi ya Mkuu wa shule (Utawala) itapokea **taarifa za dharura za wanafunzi kama vile msiba au tatizo kubwa la kifamilia pamoja na maagizo yote ya wazazi/walezi kwa mwanafunzi.**

b) Katika utoaji wa taarifa za ugonjwa na matatizo mengine, Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu popote bila idhini ya ofisi ya Mkuu wa shule ikishirikiana na ofisi ya malezi, ili kuepuka upelekaji wa taarifa zisizo sahihi kwa wazazi.

c) Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anaruhusiwa kumwombea ruhusa kama kuna tatizo. Pia ndiye atakayekuja shuleni pindi atakapohitajika kufanya hivyo.

d) Wanafunzi wanaruhusiwa kuingia ofisi yoyote shuleni isipokuwa ni lazima wagonge/ wapige hodi kabla ya kuingia.

e) Barua za wanafunzi zitapokelewa na mwalimu wa zamu ambaye atazikabidhi kwa kiranja wa zamu ili azigawe kwa wahusika.

f) **Wakati wa kufunga na kufungua shule, wanafunzi wote wataondoka kwa pamoja kwa usafiri utakaoratibiwa na shule. Hakuna ruhusa yeyote itakayotolewa mapema kabla ya siku rasmi ya kufungua na kufunga shule.**

g) Kila mwaka kutakuwa na **kikao cha wazazi** shuleni kujadili maendeleo ya shule kwa ujumla. Kikao hicho **kitafanyika tarehe 25 Septemba kila mwaka**, hivyo kila mzazi hupaswa kuhudhuria kikao hicho**.**

**12. MAMBO YASIORUHUSIWA KUFANYWA.**

a) Uasherati na uzururaji.
b) Wizi.
c) Kuchezea au kuharibu bendera ya taifa.
d) Kugoma.
e) Kumpiga au kumtukana mwalimu/mfanyakazi.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kutoroka shule au kuachana na wenzako wakati unapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
h) Kunywa au kulewa pombe/kuvuta sigara.
i) Kupigana.
j) Kupiga kelele ovyo au kuita kwa sauti kubwa (kupayuka).
k) Ubaguzi wa aina yeyote.
l) Kuzungumza lugha nyingine yoyote isipokuwa kiingereza (Kiswahili kinaruhusiwa katika mazingira maalumu tu).
m) Kuvaa mavazi yasiyo sare ya shule.
n) Kutofika au kuchelewa **sehemu ya Kusanyiko**.
o) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na simu, kamera pamoja na redio shuleni. **Shule haina dhamana ya kutunza simu**.
p) Mwanafunzi anatakiwa kuja na namba mbili za simu ambazo zitasaidia kupata mawasiliano ya wazazi/walezi wake.

q) Mwanafunzi **haruhusiwi kubadilisha dini/dhehebu awapo shuleni**. Kumbuka shule hii ni ya serikali na si ya dini/dhehebu fulani, inazingatia katiba ya nchi kuhusu uhuru wa

kuabudu, hivyo **imepanga vipindi viwili vya dini siku ya Jumatano saa 7.30 mchana mpaka saa 8.30 mchana na kila siku usiku kuanzia saa 1.30 usiku mpaka saa 2.00 usiku**. Mwanafunzi **haruhusiwi kuanzisha ratiba yake**. **Tofauti na hapo mzazi au mlezi anashauriwa kumtafutia binti yake shule ya seminari endapo mwanafunzi huyo ataonekana na wito wa dini husika**. Hii ni kuepusha usumbufu na migogoro isiyokuwa ya lazima.

r) Ni marufuku kumruhusu mgeni kufika maeneo ya bwenini.
s) Mwanafunzi **haruhusiwi kusuka nywele wala kunyoa kipara**. Mwanafunzi anapaswa kuwa na nywele fupi kuwezesha kijiti cha kiberiti kuonekana.

t) Mwanafunzi anatakiwa **aheshimu bendera ya taifa**, na ajue vema kuimba **wimbo wa Taifa**, **wimbo wa shule**, **wimbo wa Tanzania Tanzania nakupenda kwa moyo wote**, na **Tazama Ramani** (Kila mwanafunzi anapaswa kuzijua kuziimba nyimbo hizi vema).
u) **Kufanya udanganyifu kwenye mitihani** (Examination cheating case).

v) Kwa wanafunzi wanaotokea KATAVI, mwisho wa kuripoti shuleni ni saa 10.00 jioni.

## 13. ADHABU.

Adhabu zitatolewa kulingana na uzito wa makosa yaliyofanyika, **ISIPOKUWA MWANAFUNZI AKIFANYA MAKOSA YAFUATAYO ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA: -**

**I. UASHERATI NA USHOGA**
**II. UZURURAJI**
**III. WIZI**
**IV. ULEVI**
**V. UTORO (KUTOONEKANA ENEO LA ROLL CALL)**
**VI. KULALA NJE YA SHULE**
**VII. UVUTAJI WA BANGI**
**VIII. MAKOSA YA JINAI**
**IX. KUPIGANA AU KUPIGA**
**X. KUHARIBU KWA MAKUSUDI MALI YA UMMA**
**XI. KUDHARAU BENDERA YA TAIFA**
**XII. KUOLEWA**
**XIII. KUPATA MIMBA**
**XIV. KUTOA MIMBA**
**XV. UBAKAJI**
**XVI. KUGOMA, KUCHOCHEA NA KUONGOZA AU KUVURUGA AMANI NA USALAMA WA SHULE AU WATU.**
**XVII. KUKATAA ADHABU KWA MAKUSUDI**
**XVIII. KUMILIKI AU KUKUTWA NA SIMU YA MKONONI NA/AU VIAMBATA VYAKE KAMA CHARGER, LINE, EARPHONE, HEADPHONE NA REDIO.**

Elewa kuwa si rahisi kutunga sheria za kila kosa linaloweza kufanywa na mwanafunzi. Sheria ni mwongozo wa kumwelewesha mwanafunzi mambo ambayo haruhusiwi kuyafanya. Kitu muhimu ni kwamba **kila mwanafunzi atumie akili yake na busara kuweza kujua namna gani ya kuishi na walimu pamoja na wanafunzi wenzake** ili kutumia nafasi yake kujipatia elimu na kuishi kwa raha na amani katika jitihada za kujiendeleza mwenyewe, shule pamoja na taifa zima.

Kumbuka kuwa umepata bahati kubwa kuwa kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na shule hii, kwa hali hiyo toa mchango wako katika kujenga msingi imara, sifa na mwenendo mzuri na maendeleo safi kwa shule yako ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda. Ninakutakia kila lenye Kheri katika utekelezaji wa Majukumu yako kama mwanafunzi na mwanajumuiya.

**KARIBUNI SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA**

**“MAISHA NI KUJIFUNZA”**